

Maswali ya Washiriki wa Usiku wa Taarifa wa Mpango wa Elimu ya Karama**12/11/2024****jumla ya washiriki 934 wameingia**

1. Je, matokeo ya tathmini za mpango wa elimu ya karama yataachiliwa lini na jinsi gani?
 - a. Shule za eneo na wazazi wanaweza kutarajia kupokea matokeo ya tathmini zinazotumiwa katika utaratibu wa utambuzi wa karama wa wilaya katika au kabla ya mzunguko unaofuata wa utoaji wa alama wa wilaya, baada ya tathmini za hivi majuzi za karama kufanywa.
2. Je, inachukua muda gani kupata matokeo mara baada ya mtoto kutahiniwa?
 - a. Matokeo ya mtihani yatatofautiana kwani lazima tathmini zote zipitie utaratibu wa uthibitishaji wa data kabla ya data kupakiwa kwa matumizi ya karama katika mfumo wa taarifa wa wanafunzi.
3. Je, ninawezaje kumwandaa mtoto wangu kutathminiwa vyema zaidi kwa utambuzi wa karama?
 - a. Shule za eneo zinahimizwa ziwasiliane na makundi yao husika ya jumuiya kwa kutumia mfumo wa 'calling post', tovuti na vipeperushi kuhusu vipindi vyovyote vya kufanya mitihani. Kama ilivyo na tathmini yoyote ile, inapaswa kuchukuliwa kwa uzito, na wanafunzi wanaotahiniwa wanapaswa kupata usingizi wa kutosha usiku, kula kiamsha kinywa bora, na ikiwa hawajisikii vizuri wanafaa kuwasiliana hilo na afisa ushirikiano wa karama wa shule ya eneo ili kupanga upya utoaji wa mtihani kwa mtoto wako.
4. Je, alama za MAP za msimu wa baridi au machipuko zinaweza kuchukua nafasi ya alama zao za MAP za msimu wa mapukutiko kwa ajili ya kustahiki mpango wa karama katika nyanja ya Mafanikio?
 - a. Ndiyo. Alama za MAP za mtoto ndani ya mojawapo ya vipindi vya tathmini zinaweza kutumika katika kuzingatia utambuzi wa karama.
5. Je, wazazi watapokea vipi matokeo ya tathmini za MAP kwa mtoto wao katika Msimu wa Mapukutiko, Baridi na Machipuko?
 - a. Mwalimu wa mtoto wako anaweza kutoa matokeo ya MAP katika kila kipindi cha tathmini. Mshauri na mwalimu mkuu/mwakilishi wa shule ya mtoto wako anaweza kutoa matokeo ya MAP pia. Kalenda ya Tathmini ya Shule za Kaunti ya DeKalb inaweza kupatikana kwenye kiungo hiki: <https://dekalbschoolsga.blob.core.windows.net/wpcontent/2024/07/2024-2025-Dekalb-County-School-District-Assessment-Calendar-1.pdf>
6. Je, wazazi wanaarifiwaje kuhusu mitihani zaidi? (mfano: Asilimia 75-98 —> ITBS)
 - a. Afisa ushirikiano wa mpango wa karama wa shule ya eneo atatuma nyumbani Fomu ya Idhini ya Mzazi ya Kutathmini inayoomba ruhusa kwa shule kufanya tathmini zaidi ili kuzingatiwa kwa huduma za karama.

7. Je, ninawezaje kupata maelezo zaidi kuhusu miundo ya huduma za karama ndani ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb?
 - a. Maelezo ya miundo ya huduma za karama yanaweza kukaguliwa kwenye kiungo hiki (kichupo cha “programs” (mipango)): <https://www.dekalbschoolsga.org/gifted/>
8. Mtoto wetu yuko katika mpango wa karama lakini hana mwalimu aliyeidhinishwa wa karama. Je, ni aina gani ya huduma za karama anapaswa/atakuwa anapata?

Wanafunzi wanaopokea huduma za karama wanapaswa kufundishwa na mwalimu aliye na cheti cha karama au mwalimu ambaye amejandikisha katika mpango wa uidhinishaji wa karama. Fahamu kwamba huenda wanafunzi wasipate huduma za karama katika masomo yote. Wanaweza kupokea huduma za karama katika sehemu moja tu ya siku. Wasiliana na afisa ushirikiano wa karama wa shule yako ili upate maelezo zaidi kuhusu jinsi mtoto wako anavyohudumiwa.
9. Ikiwa mtoto wangu anatahiniwa kwa mpango wa karama, tunaweza kuwasiliana na nani ili kujua kama alikidhi masharti?
 - a. Arifa kwa Mzazi/Mlezi hutolewa na shule ya eneo. Wazazi wanaweza kutarajia kupokea matokeo ya tathmini zinazotumiwa katika utaratibu wa utambuzi wa karama wa wilaya katika au kabla ya mzunguko wa utoaji wa alama wa wilaya. Hati zitajumuisha barua ya ustahiki, Makubaliano ya Kuendelea, Ripoti ya Alama za Mwanafunzi/Mtu Binafsi, na ripoti ya ustahiki ya hali ya karama.
10. Je, Kaunti ya DeKalb inaunga mkono kuruka gredi ikiwa mpango wa karama katika shule hautoshi?
 - a. Iwapo mzazi/mlezi anataka kujadili uharakishaji wa gredi au kuruka gredi kwa mtoto wao, anapaswa kuwasiliana na mwalimu mkuu wa shule ya mtoto wao. Utaratibu wa uharakishaji wa gredi hauko chini ya usimamizi wa Idara ya Elimu ya Karama. Utaratibu huu upo katika ngazi ya shule ya eneo kwa kushirikiana na **Sera ya IHEB ya Bodi ya DCSD: Mafanikio ya Kimasomo:**
<https://simbli.eboardsolutions.com/Policy/ViewPolicy.aspx?S=4054&revid=7r6KfX9meCnEdUJeDhccVQ==&st=grade%20acceleration&mt=Exact>
11. Je, mtoto aliye katika shule ya kabla ya chekechea (Pre-K) anaweza kustahiki kupata elimu ya karama?
 - a. Hapana. Elimu ya Karama ndani ya shule za umma za Jimbo la Georgia hutathminiwa, kutolewa, na kufadhiliwa kuanzia darasa la Chekechea hadi gredi ya 12.
12. Je, ni nini kinatumika kubaini ni aina gani ya muundo wa mpango wa karama inayotolewa katika kila shule?

- a. Uongozi wa shule ya eneo una uhuru wa kubaini ni miundo ipi ya utoaji inayokidhi kwa njia bora zaidi mahitaji ya wanafunzi wake wenye karama na kuendana uwezo wa wafanyakazi wao. Hii itatofautiana kulingana na shule. Timu ya Wilaya ya Elimu ya Karama inaendelea kupatikana kwa wasimamizi wa shule ili kuwasaidia katika kuchagua muundo wa utoaji wa huduma za karama katika shule ya eneo, kwa kuzingatia mambo ya ndani (yaani, idadi ya wanafunzi waliotambuliwa kwa karama, walimu walioidhinishwa kwa karama, ratiba ya shule, n.k.)
13. Je, unapendekeza wazazi wafanye nini ili kuhakikisha shule inawafahamisha na kuwaarifu wazazi katika utaratibu huu mzima?
- a. Shule za eneo zinahimizwa ziwasiliane na makundi yao husika ya jumuiya kwa kutumia mfumo wa 'calling post', tovuti na vipeperushi kuhusu vipindi vyovyote vya kufanya mitihani. Wazazi wanahimizwa wawasiliane na afisa ushirikiano wa karama wa shule ya eneo kwa maswali yoyote mahususi yanayohusiana na utaratibu wa mitihani ya karama.
14. Baada ya mtoto wako kutahiniwa, tunaweza kutarajia nini?
- a. Baada ya utaratibu wa utambuzi wa karama umekamilika na seti za data inayotumika katika utaratibu huu kuhifadhiwa katika Mfumo wa Taarifa za Mwanafunzi (SIS), arifa ya mzazi/mlezi hutumwa na shule yako ya eneo. Wazazi wanaweza kutarajia kupokea matokeo ya tathmini zinazotumiwa katika utaratibu wa utambuzi wa karama wa wilaya katika au kabla ya mzunguko wa utoaji wa alama wa wilaya. Hati zitajumuisha barua ya ustahiki, Makubaliano ya Kuendelea, Ripoti ya Alama ya Mwanafunzi/Mtu Binafsi, Brosha ya Shule ya Eneo, na ripoti ya ustahiki ya hali ya karama. Je, iwapo atatambuliwa kama mwenye karama ni mabadiliko gani yatafanywa katika elimu yake? Viongozi wa shule hufanya matembezi ya uchunguzi wa mafundisho ya mara kwa mara, uchunguzi usio rasmi na rasmi wa wafanyakazi ili kubaini kiwango cha ushiriki wa wanafunzi na kuweka alama kazi walizopewa. Mwalimu hupewa maoni yaliyoandikwa ili kufanya marekebisho yanayofaa ya mpango wa somo. Idara ya Elimu ya Karama inatoa usaidizi kwa wasimamizi na walimu wa shule za eneo kwa kutoa mafunzo ya kitaaluma wakati wa msimu wa kiangazi na wakati wa shule yanayohusu mada kama vile urekebishaji, mikakati ya kufundisha na kuunda mazingira yenye changamoto za kimasomo. Je, atahamia shule tofauti? Hapana. Ingawa baadhi ya wazazi wanaweza kuchagua kushiriki katika Mpango wa Kujiandikisha katika Chaguo la Shule, hii ni ya hiari na si sawa na utambuzi wa karama.
15. Je, Wilaya inafanya nini kutoa mafunzo ya ukuaji na maendeleo kwa Walimu ambao wanaweza kuwa wanafundisha watoto wenye karama katika kozi ambazo hazichukuliwi kuwa za karama/kina.
- a. Idara ya Elimu ya Karama inatoa mafunzo ya kitaalamu kwa walimu wote katika msimu wa kiangazi na wakati wa mwaka mzima wa shule. Vipindi hivi vinashughulikia uundaji wa mazingira yenye changamoto za kimasomo kupitia mada kama vile mawazo ya kuhoji/majadiliano na utoaji wa maoni/ukuaji. Viongozi wa shule pia huchunguza mara kwa mara madarasa ndani ya shule zao, ya wanafunzi wa karama na vinginevyo, na kuwapa

walimu maoni, fursa za kujiendeleza kitaaluma, na tathmini zinazohusiana na ufanisi na ubora wa mafundisho ya darasani na wanaweza pia kuchagua kuwa na kipindi cha mafunzo maalum ambacho kinaweza kukidhi vyema zaidi mahitaji ya wafanyakazi wao.

16. Ikiwa mwanafunzi wangu anastahiki huduma za karama, huduma hizo zitaanza lini?
 - a. Wazazi wanaweza kutarajia wanafunzi wao kuanza kupokea huduma za karama katika muhula/mwaka unaofuata wa masomo kulingana na wakati ustahiki umebainishwa. Wanafunzi wanaochukuliwa kuwa wanastahiki huduma za karama katika Msimu wa Machipuko wanaweza kutarajia kuhudumiwa katika Msimu wa Mapukutiko wa mwaka unaofuata wa masomo.
17. Je, kuna njia yoyote ya kuangalia hali ya sasa ya karama ya mtoto wangu?
 - a. Shule ya eneo hutoa arifa kwa wazazi ambao mtoto wao anachunguzwa kwa huduma za karama. Hii itajumuisha ripoti za alama binafsi za mtoto na ripoti ya ustahiki inayoonyesha hali yake ya karama.
18. Je, elimu ya karama ina athari gani kwa wanafunzi ambao wana mpango wa IEP?
 - a. Marekebisho yoyote yaliyotajwa katika Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) au Mpango wa 504 lazima yafuatwe katika kuhakikisha mwanafunzi anafanya mtaala na/au viwango vya masomo vinavyofundishwa.
19. Ikiwa mtoto wangu alistahiki kupata elimu ya karama katika shule ya msingi, na amedumisha hali ya karama, je, utambuzi huo wa karama utaendelea hadi shule ya kati na sekondari?
 - a. Ndiyo. Mara tu mwanafunzi anapostahiki huduma za karama, hakuna tathmini zaidi inayohitajika ili kubaki kwenye mpango wa karama.
20. Je, nini tofauti na mtaala wa jumla kwa wanafunzi wanaopokea huduma za karama?
 - a. Kulingana na Kanuni ya 160-4-2-.38 ya MPANGO WA ELIMU KWA WANAFUNZI WENYE KARAMA ya Idara ya Elimu ya Georgia, Mtaala Uliorekebishwa unamaanisha kuwa “kozi za masomo ambazo maudhui, mikakati ya kufundisha, na matarajio ya ustadi wa mwanafunzi yamerekebishwa ili yamfae wanafunzi wenye karama.” <https://cdn-cms-gadoe-org-fpf4gke0fwd4htef.a03.azurefd.net/app/uploads/2024/11/EDUCATION-PROGRAM-FOR-GIFTED-STUDENTS.pdf>
21. Baada ya wanafunzi kutambuliwa kuwa na karama, Wilaya inafuatiliaje na kutathmini msaada wanaopata?
 - a. Idara ya Elimu ya Karama ya DCSD kwa sasa inajumuisha Waratibu Wakuu wawili wa Elimu ya Karama. Waratibu hawa hutembelea shule mara kwa mara na wanawasiliana mara kwa mara na walimu wa karama, maafisa wa ushirikiano wa karama, na wasimamizi wa shule kuhusu mahitaji, vipengele, maendeleo ya kitaaluma, tathmini za utambuzi na mafundisho ya darasani ya mpango wa karama. Aidha, katika ngazi za Wilaya na shule, tathmini zetu za MAP

- huripoti matokeo ya jumla mara tatu kwa mwaka wa masomo kuhusu ukuaji na matokeo ya jumla ya masomo ya wanafunzi wetu wa karama – kwa ufuatiliaji wa athari za usaidizi huo.
22. Je, ni nyenzo zipi za ziada za kufundisha ambazo walimu wa sehemu za kozi za karama wataweza kuzifikia?
- a. Kwa upande wa nyenzo za kufundisha kwa walimu wanaofundisha sehemu za karama, Idara ya Elimu ya Karama inapendekeza vitabu na nyenzo za mtandaoni ili kuwasaidia walimu wa karama katika kuwasaidia wanafunzi wanapoendelea kukuza ujuzi wa kufikiri na kuchanganua. Nyenzo za ziada za mafundisho zinatarajiwa kununuliwa katika mwaka wa masomo wa 2024-2025- na walimu watapewa mafunzo ya kina kuhusu utekelezaji na matumizi yake ifaayo pindi zitakapopatikana.
23. Je, ni wapi kwenye tovuti ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb tunaweza kupata maelezo kuhusu Elimu ya Karama?
- a. www.DeKalbSchoolsGA.org/Gifted
24. Ikiwa mtoto wangu ana alama za kustahiki katika angalau moja ya tathmini za karama, je, ni lazima afanye tathmini kama hiyo tena ili kuzingatiwa kwa utambuzi wa karama baadaye?
- a. Hatafanya hivyo ndani ya muda wa miaka miwili kwa tathmini hiyo sawa. Alama ni halali kwa miaka miwili kwenye tathmini mahususi kwa mwanafunzi ili hatimaye astahiki kwa huduma za karama katika nyanja zingine zinazohitajika (yaani mafanikio, uwezo wa kiakili, ubunifu, motisha)
25. Je, mwanafunzi anaweza kutathminiwa kupata elimu ya karama katika mazingira ya shule ya kibinafsi?
- a. Hapana. Wanafunzi lazima waandikishwe na wahudhurie Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb ili kushiriki katika utaratibu wa tathmini ya karama.
26. Je, mwanafunzi anaweza kutathminiwa kwa utambuzi wa karama tena wakati wa kipindi kingine cha tathmini ikiwa hatastahiki mara ya kwanza?
- a. Ndiyo. Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb hutumia vipindi viwili tofauti vya kutathmini utambuzi wa karama wakati wa mwaka wa masomo: Msimu wa Mapukutiko (Oktoba) na Machipuko (Februari)
27. Je, mwanafunzi aliyetambuliwa kuwa na karama anaweza kuruka gredi?
- a. Uamuzi huu hufanya kulingana na mwanafunzi, na unashughulikiwa katika ngazi ya shule kwa kushirikiana na familia ya mwanafunzi. Utambuzi wa karama hauathiri utaratibu wa uharakishaji wa gredi unaowezekana kwa mwanafunzi. Iwapo mzazi/mlezi anataka kujadili uharakishaji wa gredi au kuruka gredi kwa mtoto wao, anapaswa kuwasiliana na mwalimu mkuu wa shule ya mtoto wao. Utaratibu wa uharakishaji wa gredi hauko chini ya usimamizi wa Idara ya Elimu ya Karama. Utaratibu huu upo katika ngazi ya shule ya eneo kwa kushirikiana na **Sera ya IHEB ya Bodi ya DCSD: Mafanikio ya Kimasomo:**

<https://simbli.eboardsolutions.com/Policy/ViewPolicy.aspx?S=4054&revid=7r6KfX9meCnEdUJeDhccVQ==&st=grade%20acceleration&mt=Exact>

28. Je, ni zipi baadhi ya faida za kutambuliwa kuwa na karama?
- Faida za utambuzi wa karama zinajumuisha, lakini sio tu, kuongezeka kwa fursa kwa wanafunzi kuwa pamoja na wenzao wenye malengo sawa, mafundisho kwa kasi ya haraka ili kukidhi mahitaji yao ya kufundishwa, mafundisho kulingana na uwezo na/au mapendeleo ya wanafunzi, kupokea mafundisho kutoka kwa mwalimu mwenye cheti/aliyeidhinishwa kwa karama ambaye amefunzwa kutambua mahitaji ya kipekee ya wanafunzi wenye karama kwa kutoa kazi za wazi zinazochochea kufikiri kwa makini, ubunifu, na kutatua matatizo ambayo inaweza kusababisha kuongezeka kwa fursa za ziada za masomo kwa wanafunzi. Zaidi ya hayo, katika ngazi ya shule ya upili, huduma za karama kwa ujumla hutolewa kupitia uratibu wa kozi za Advanced Placement (AP).
29. Je, kuhudhuria kunaathiri ustahiki wa mpango wa karama?
- Sio moja kwa moja. Hata hivyo, ikiwa mwanafunzi hayupo shuleni mara kwa mara na hivyo anakosa mafundisho muhimu ya darasani, hii itaathiri utendaji wake wa kimasomo, jambo linaloweza kuathiri matokeo yake kwenye tathmini mbalimbali za utambuzi wa karama.
30. Je, kuna nyenzo za ziada za elimu kwa wanafunzi wenye karama nje ya mafundisho ya darasani na miundo ya huduma ambazo kila shule inaweza kutumia?
- Kuna nyenzo nyingi zinazopatikana kwa wanafunzi kupitia Clever/Launchpad. Nyenzo zinazopendekezwa ni pamoja na GALILEO na MackinVia ambazo zote zinatoa Vitabu pepe kwa gredi zote. Pia kuna matukio mengi yanayotolewa na wilaya ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu: Mpango wa Governor's Honors, Matukio ya Kituo cha Sayansi cha Fernbank, Tech for Littles: Maonyesho ya Teknolojia ya Byte Sized Brilliance ya DeKalb, Siku ya Kitaifa ya Historia, Maonyesho ya Teknolojia ya DeKalb, Helen Ruffin Reading Bowl, Maonyesho ya Sayansi, na Maonyesho ya Masomo ya Jamii.
31. Je, mzazi/mlezi anapaswa kuwasiliana na nani ikiwa haelewi au hajaridhika na huduma za elimu ya karama zinazotolewa kwa mtoto wao darasani?
- Katika hali kama hizi, inashauriwa uwasiliane na mwalimu moja kwa moja ili kujadili hili zaidi. Ikiwa mzazi/mlezi hawezi kumfikia au hajaridhika na mawasiliano kutoka kwa mwalimu kuhusu suala hilo, mzazi/mlezi anaweza kuwasiliana na mwalimu mkuu wa shule. Ikiwa mzazi hawezi kumfikia au hajaridhika na mawasiliano kutoka kwa ofisi ya mwalimu mkuu wa shule, mzazi/mlezi anaweza kuwasiliana na ofisi ya msimamizi mkuu wa eneo la shule.
32. Je, utambuzi wa karama ni halali kwa kaunti nzima katika shule tofauti. Je, utambuzi utakuwa halali endapo mtoto anahama shule?

- a. Ndiyo. Ikiwa mwanafunzi amestahiki kupata huduma za elimu ya karama ndani ya shule yoyote ya umma katika Georgia, utambuzi huu utahamishwa naye hadi shule nyingine yoyote ya umma katika Georgia.
33. Je, wazazi wanaweza kujiamulia wenyewe ikiwa mtoto wao ataandikishwa katika sehemu/kozi zilizotambuliwa za karama?
- a. Ingawa mzazi hawezi kujiamulia mwenyewe ikiwa mtoto wake atatambuliwa kwa huduma za karama, wazazi wanashauriwa kila mara wawasiliane na mshauri na/au mwalimu mkuu/mwakilishi wa shule ya mtoto wao ili kutoa maoni kuhusu mazingira ya masomo, ratiba na maendeleo ya shule ya mtoto wao.
34. Ikiwa mwanafunzi anakidhi masharti ya kustahiki mpango wa karama, ahame na kisha arudi katika Georgia, je, atahitaji kutumwa tena au kutathminiwa upya kwa huduma za karama?
- a. Hapana. Utambuzi wake wa awali wa mpango wa karama ndani ya Jimbo la Georgia utaendelea kutumika.
35. Je, shule za mkataba zinapata usaidizi sawa na shule za umma katika Kaunti ya DeKalb?
- a. Idara yetu ya Uvumbuzi wa Shule ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb hutoa usaidizi na inawasiliana mara kwa mara na shule za mkataba zilizoidhinishwa na Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb – kwa ushirikiano na Idara nyingi.
<https://www.dekalbschoolsga.org/charter-schools/>
36. Je, Elimu ya Karama katika Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb ina uhusiano wowote wa moja kwa moja na shule za magnet/mipango ya magnet?
- a. Kwa ufupi, hapana. Ingawa mara nyingi wanafunzi walioandikishwa katika mipango ya magnet ya DCSD hutambuliwa kuwa na karama na hupokea huduma za karama ndani ya shule za magnet, huduma za elimu ya karama hazihusiani na shule za magnet wala mipango ya magnet. Idara ya Elimu ya Karama haisimamii shule za magnet au mipango ya magnet katika Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb. Maelezo zaidi kuhusu chaguo za mipango ya magnet katika Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb yanaweza kupatikana kwenye kiungo hiki: <https://www.dekalbschoolsga.org/school-choice/>
37. Je, Idara ya Elimu ya Karama ina jukumu gani katika kusaidia shule kubainisha miundo ya huduma za karama wanayotumia katika madarasa ya karama?
- a. Waratibu Wakuu wa Elimu ya Karama wanapatikana ili kukutana na wasimamizi wa shule ili kujadili miundo hii. Wasimamizi wa shule huamua miundo inayofaa zaidi kwa shule zao.
38. Je, mtaala unapaswa kutofautiana vipi ndani ya madarasa ya karama kwa wanafunzi wenye karama?
- a. Kulingana na Kanuni ya 160-4-2-.38 ya MPANGO WA ELIMU KWA WANAFUNZI WENYE KARAMA ya Idara ya Elimu ya Georgia, Mtaala Uliorekebishwa unamaanisha kuwa “kozi za masomo ambazo maudhui, mikakati ya kufundisha, na matarajio ya ustadi wa mwanafunzi

yamerekebishwa ili yamfae wanafunzi wenye karama.” <https://cdn-cms-gadoe-org-fpf4gke0fwd4htef.a03.azurefd.net/app/uploads/2024/11/EDUCATION-PROGRAM-FOR-GIFTED-STUDENTS.pdf>

39. Je, kaunti inadhibitisha vipi, na kwa kipimo gani, kwamba shule kwa kweli inafuata mwongozo wa mpango wa karama wa kaunti?
 - a. Kuna hatua kadhaa za ukaguzi wakati wa mwaka wa masomo ambapo viongozi lazima wathibitishe miundo ya huduma ya karama iliyotumiwa na shule yao ili kuripoti utiifu wa masharti kwa Idara ya Elimu ya Georgia. Idara yetu ya Elimu ya Karama (Waratibu Wakuu wawili kwa sasa kufikia Msimu wa Mapukutiko wa 2024) hutembelea shule mara kwa mara, hutoa maendeleo ya kitaaluma kuhusu elimu ya karama shuleni, na mara kwa mara huwasiliana na kushirikiana na viongozi wa shule kuhusu masuala yanayohusu elimu ya karama. Pia kuna ushirikiano na mawasiliano ya mara kwa mara na Ofisi za Wasimamizi Wakuu wa Maeneo kuhusu masuala ya elimu ya karama ndani ya shule.
40. Je, kuna faida yoyote kwa wanafunzi wenye karama katika uandikishaji wa chuo kikuu?
 - a. Ingawa kila mfumo wa chuo kikuu una masharti yake ya uandikishaji, ni kawaida kwamba ndani ya shule za umma za Georgia, huduma za karama hutolewa kwa wanafunzi wa shule ya upili kupitia kozi za Advanced Placement (muundo wa huduma za maudhui ya hali ya juu). Kozi za Advanced Placement (AP) kwenye hati za alama za shule ya upili za mtoto kwa kawaida hufanya maombi yao ya chuo yawe na ushindani zaidi.
41. Ikiwa mtoto yuko katika mpango wa karama, atakwenda darasa tofauti kupata huduma au mwalimu wa karama atamhudumia mtoto darasani mwao?
 - a. Hii itategemea muundo wa huduma ya karama ambao shule hutumia. Uamuzi huu unatolewa katika ngazi ya shule kulingana na mahitaji, idadi ya wanafunzi, wafanyakazi wa shule ya eneo, n.k.
42. Je, Wilaya inapokea aina yoyote ya ufadhili inayohusiana na idadi ya wanafunzi wenye karama katika kila shule?
 - a. Katika mwaka wa masomo wa 2024-2025, wilaya za shule za umma ndani ya Jimbo la Georgia hupata uandikishaji wa muda wote (full time enrollments, FTE) wa 1.7340 kwa kila sehemu ya mafundisho ya mwanafunzi aliyetambuliwa kuwa na karama ambamo anahudumiwa na mwalimu aliyeidhinishwa ndani ya muundo wa huduma ya kipawa ulioidhinishwa. FTE hupangwa na kuripotiwa kwa Idara ya Elimu ya Georgia kila Oktoba na Machi. <https://georgiainsights.gadoe.org/Data-Collections/Documents/FTE%20Resources/FY2025/FY2025%20FTE%20Categories%20and%20Weights.pdf>
43. Ikiwa mwanafunzi anastahiki kupata elimu ya karama, anaanza lini huduma zake za karama?
 - a. Wazazi wanaweza kutarajia wanafunzi wao kuanza kupokea huduma za karama katika muhula/mwaka unaofuata wa masomo kulingana na wakati ustahiki umebainishwa. Kwa

mfano, wanafunzi wanaochukuliwa kuwa wanastahiki huduma za karama katika msimu wa Machipuko wanaweza kutarajia kuhudumiwa katika msimu wa Mapukutiko wa mwaka unaofuata wa masomo.

44. Je, mwanafunzi anaweza kutathminiwa kupata elimu ya karama katika miaka kadhaa mfululizo ya masomo?
 - a. Ndiyo. Mwanafunzi anaweza kutathminiwa kwa utambuzi wa karama katika miaka kadhaa ya masomo kwa mfululizo. Ikiwa mwanafunzi atapata alama ya kustahiki kwa mojawapo ya vikoa vinne (Mafanikio, Uwezo wa Akili, Ubunifu, Motisha), alama ya kustahiki zitakuwa halali kwa miaka miwili kuanzia tarehe ya tathmini.
45. Mara baada ya mwanafunzi kutambuliwa kuwa mwenye karama, je, anahitaji kutathminiwa mara kwa mara ili kuhakikisha bado anastahiki, au anastahili kupata huduma za karama hadi atakapohitimu?
 - a. Mara mwanafunzi anapostahiki kupata huduma za karama ndani ya wilaya ya shule ya umma ya Georgia, hahitaji kutathminiwa tena ili kuendelea kustahiki kupata huduma za karama.
46. Kwa wanafunzi wa shule ya kati, mpango wa Karama hutumiwaje hadi Shule ya Upili na pia unaingiliana vipi na mpango wa International Baccalaureate?
 - a. Idara ya Elimu ya Georgia huidhinisha kozi za mpango wa Advanced Placement na kozi za International Baccalaureate ili kustahiki kutumika kama miundo ya huduma za elimu ya karama inayoruhusiwa, mradi tu mwalimu wa kozi hiyo ameidhinishwa kwa mpango wa karama. Katika shule ya upili, muundo bora zaidi wa huduma ya karama ni kozi za Advanced Placement.
47. Ikiwa IEP ya mwanafunzi wangu inasema kwamba anapata mitihani ya kikundi kidogo, au marekebisho mengine ya mitihani je, haya yanatumika kwa mitihani ya karama?
 - a. Katika hali kama hizi, IEP ya mwanafunzi itazingatiwa kwa njia ya Wilaya kutambua mbinu za utathmini wa karama zilizoidhinishwa na Idara ya Elimu ya Georgia ambapo marekebisho ya mitihani ya IEP ya mwanafunzi hayaathiri alama au kanuni za tathmini. Uamuzi huu utategemea mwanafunzi, kulingana na ustahiki wa mtoto kwa huduma za elimu maalum na marekebisho ya mitihani yaliyomo ndani ya IEP ya mtoto.
48. Je, tathmini sanifu ndiyo njia pekee ya mwanafunzi kustahiki mpango wa karama?
 - a. Sheria za Idara ya Elimu ya Georgia zinahitaji kwamba ili mwanafunzi aweze kustahiki huduma za karama, ustahiki katika angalau kiko kimoja cha Mafanikio na/au Uwezo wa Akili lazima ubainishwe na matokeo ya zana iliyoidhinishwa ya utathmini. Maelezo zaidi kuhusu ustahiki yanaweza kupatikana kwenye kiungo hiki (kichupo cha “eligibility” (ustahiki)): <https://www.dekalbschoolsga.org/gifted/>
49. Je, mwanafunzi aliye na IEP anaweza kustahiki kupata mpango wa karama?

- a. Ndiyo. Masharti ya ustahiki kwa elimu ya karama ni sawa kwa wanafunzi wote ndani ya Jimbo la Georgia. Maelezo zaidi kuhusu ustahiki wa karama yanaweza kupatikana kwenye kiungo hiki (kichupo cha “eligibility” (ustahiki)): <https://www.dekalbschoolsga.org/gifted/>

50. Je, huduma za karama zinapaswa kutolewa kwa kiwango gani cha chini zaidi kinachohitajika kila wiki?

- a. Huduma za karama zinapaswa kutolewa kwa kiwango cha chini zaidi cha sehemu 5 za mafundisho kwa wiki (takriban dakika 50 kwa kila sehemu) – ili shule ipate uandikishaji wa muda wote wenye karama (FTE) kwa kila mwanafunzi aliyetambuliwa kuwa na karama.

51. Je, kuna manufaa yoyote ya ziada ya mafundisho kwa walimu wa elimu ya jumla ili kupata uidhinishaji wao wa karama?

- a. Kabisa! Mikakati madhubuti hufanya kazi kwa wanafunzi wote. Mpango huu umeundwa kwa ajili ya walimu wa DeKalb na unaangazia nyenzo zinazotolewa na wilaya. Walimu hujifunza mikakati na wanaombwa kuitumia darasani. Walimu pia hunufaika kutokana na ushirikiano na wenzao shuleni na katika wilaya nzima.

52. Je, Elimu Maalum, Sehemu ya 504, na Elimu ya Karama hufanyaje kazi pamoja?

- a. Mwanafunzi aliye na IEP (elimu maalum) au Mpango wa Sehemu ya 504 anaweza kustahiki huduma za elimu ya karama. Pindi anapofanya hivyo, anasalia kustahiki kupata mabadiliko na marekebisho yoyote ndani ya Mpango wao wa IEP au Sehemu ya 504 katika mazingira ya mafundisho ya karama, na huduma nyinginezo za elimu maalum zilizo ndani ya IEP yake.

53. Je, elimu ya karama inazingatia maeneo yoyote kama vile STEM, sanaa, n.k?

- a. Inaweza. Lengo la mafundisho ya huduma za karama linategemea maamuzi ya mwalimu na shule. Hali ya utambuzi wa karama inawezesha mtoto wako kuhudumiwa na mwalimu aliyeidhinishwa wa karama. Wanafunzi hupokea mtaala uliorekebishwa ambao GaDOE inafafanua kama “kozi za masomo ambapo maudhui, mikakati ya ufundishaji, na matarajio ya ustadi wa wanafunzi yamerekebishwa ili kuwafaa wanafunzi wenye karama.” Kuwa na utambuzi wa huduma za karama hakuathiri uwekaji wa mtoto shuleni ndani ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD). Kila shule ya DCSD inapaswa kutoa huduma za elimu ya karama kwa wanafunzi wanaostahiki.

54. Je, data kuhusu idadi ya wanafunzi wenye karama kulingana na kila gredi inapatikana hadharani?

- a. Kitengo cha Utafiti na Uwajibikaji cha Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb hudhibiti dashibodi zetu za data inayotolewa hadharani kwenye tovuti hii: <https://www.dekalbschoolsga.org/data-dashboards/>. Tunapanga kuchapisha data ya ushiriki wa mpango wa Karama ya Wilaya yetu katika siku za usoni kwenye tovuti hiyo.

55. Je, ninaweza kuwasiliana na nani ikiwa nina maswali kuhusu tathmini za karama?

- a. Shule ya mtoto wako ina afisa maalum wa ushirikiano. Mwalimu mkuu/mwakilishi wa shule yako anapaswa kuwa na uwezo wa kutambua na kukuunganisha na afisa ushirikiano wa

karama wa shule. Mratibu Mkuu wa Elimu ya Karama wa Wilaya anayesaidia tathmini za karama ni Bi. Donyell Atkinson. (Emmika_Atkinson@DeKalbSchoolsGA.org)

56. Je, shule zina vikomo kwa idadi ya wanafunzi wanaotambuliwa kwa elimu ya karama kila mwaka?
 - a. Hapana. Hakuna kikomo kwa idadi ya wanafunzi wanaoweza kustahiki huduma za karama kila mwaka.
57. Je, ni baadhi ya mada gani mahususi za elimu ya karama ambayo walimu wanaweza kushiriki kwa maendeleo ya kitaaluma? Na mada kama vile ukakamavu wa kitaaluma, kufikiria kwa hali ya juu, na kufikiria kwa makini zinahimizwa vipi kwa wanafunzi WOTE kupitia maendeleo kitaaluma ya elimu ya karama?
 - a. Mada ni pamoja na kuhoji, kutoa maoni, mafundisho ya kikundi kidogo, teknolojia, ubunifu, na mafunzo ya msingi wa mradi. Walimu wote wanaalikwa kushiriki katika mafunzo ya kitaaluma kutoka kwa idara ya karama.
58. Je, ufadhili wa masomo unapatikana kwa wanafunzi wenye karama baada ya kuhitimu?
 - a. Kuna aina nyingi za ufadhili wa elimu ya juu/unaoendelea zinazopatikana kwa wanafunzi kutoka mazingira na asili zote. Wasiliana na mshauri wa shule ya upili ya mwanafunzi wako kwa maelezo mahususi na usaidizi wa kupata ufadhili wa masomo unaofaa mazingira na asili ya mtoto wako. Maelezo ya ziada kuhusu usaidizi wa kifedha wa chuo ndani ya Georgia yanaweza kupatikana kwenye tovuti hii: <https://www.gafutures.org/>
59. Je, ni kwa jinsi gani walimu na wazazi wanaweza kupata maelezo zaidi kuhusu kulinda afya ya akili ya wanafunzi wenye karama?
 - a. Kitengo cha Huduma za Wrap Around hutoa nyenzo mbalimbali kwa walimu, wanafunzi na familia katika kusaidia afya ya akili ya wanafunzi. Hii inajumuisha moduli za kujifunza ujuzi wa kijamii na kihisia zinazotolewa kwa wanafunzi. Ikiwa mwalimu au mzazi anataka maelezo zaidi kuhusu masuala ya afya ya akili yanayomhusu mwanafunzi, anafaa kuwasiliana na mshauri wa shule au mfanyakazi wa jamii wa shule kwa usaidizi zaidi.
60. Je, uidhinishaji wa karama unaofuata wa mwalimu utatolewa lini?
 - a. Maombi ya mpango wa uidhinishaji wa karama hukubaliwa kila mwezi Agosti – katika wiki kadhaa za kwanza za mwaka wa masomo.
61. Je, madarasa ya sehemu za karama yana ukubwa gani?
 - a. Miongozo ya ukubwa wa darasa kwa sehemu za miundo ya huduma za karama inaweza kupatikana katika Mwongozo wa Nyenzo za Karama wa Idara ya Elimu ya Georgia, kwenye kiungo hiki (sehemu ya “services models” (miundo ya huduma)): <https://www.dekalbschoolsga.org/documents/gifted/manuals/gadoe-manual.pdf>

62. Je, kuna fursa kwa wanafunzi (wenye karama au la) kushiriki katika ukufunzi wa kazi na uzoefu mwingine wa kujifunza mahali pa kazi kupitia Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb?
- a. Ndiyo. Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb hutoa njia mbalimbali za Elimu ya Kazi, Ufundi na Kilimo (Career, Technical, and Agricultural Education, CTAE) kwa wanafunzi wa shule za upili. Maelezo zaidi kuhusu CTAE yanaweza kupatikana katika tovuti hizi:
<https://ctaedekalb.org/home>; <https://www.dekalbschoolsga.org/curriculum/high-school/>. DCSD pia huwapa wanafunzi wa shule za upili fursa nyingi za mipango ya kujifunza kupitia kazi. Idara yetu ya CTAE na wafanyakazi wa Mafunzo ya Kazi hudumisha ushirikiano na mawasiliano ya mara kwa mara na wataalamu wa elimu ya juu na sekta kuhusu matoleo, vipengele na miundo ya mipango. Uliza mshauri wa mwanafunzi wako wa shule ya upili kwa maelezo zaidi kuhusu njia ya CTAE na matoleo ya kujifunza ya kazini.